IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

# MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA *MAMAEE* NA *BEMBEAYAMAISHA*.

***Njeru Karimi Stella, Chuo Kikuu Cha Mount Kenya***

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza mabadiliko ya utambulisho wa wahusika wa kike katika tamthilia mbili zilizochaguliwa: *Mama Ee* (1987) ya Ari Katini Mwachofi na *Bembea ya Maisha* (2022) ya Timothy Arege. Utafiti ulizingatia jinsi utambulisho wa wahusika wa kike unavyojibadilisha kwa kuzingatia kipindi na jinsia ya waandishi wa tamthilia hizi. Pia, uliangazia sababu zinazochangia mabadiliko haya katika uwasilishaji wa wahusika wa kike, kwa kuzingatia mazingira ya uandishi na mitazamo ya waandishi husika. Ni wazi kuwa fasihi hupata malighafi yake kutoka kwa jamii. Ili kutimiza lengo hili, nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika iliyoanzishwa na Steady (1981) ilitumika. Utafiti huu ni wa kimaelezo na ulifanyika maktabani. Sampuli ilichaguliwa kwa kutumia mbinu za kusudi kwani ililenga vitabu maalum vya tamthilia vinavyoonyesha mabadiliko katika utambulisho wa mwanamke. Baada ya data kukusanywa, ilichambuliwa kwa njia ya kimaelezo kulingana na mihimili ya nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika pamoja na malengo ya utafiti huu ambayo ni; kuchanganua utambulisho wa kike kisanii katika tamthilia za waandishi hawa wawili, kuchunguza athari za mazingira katika utambulisho wa kike katika tamthilia teule, na kubainisha athari za mitazamo ya waandishi hawa katika usawiri. Sura ya kwanza niutangulizi wa utafiti, ambapo mada ya utafiti, umuhimu wa utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti huu zimeshughulikiwa Sura ya pili inayoshughulikiamapitio ya maandiko kuhusu mada na misingi ya kinadharia iliyoongoza utafiti huu imejadiliwa. Katika sura ya tatu, muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadilengwa, uteuzi wa sampuli, ukusanyajidata, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo na maadili ya utafiti zimeshughulikiwa. Sura ya nne ni uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Ile ya mwisho ni matokeo na mapendekezo ya utafiti huu.

## Utangulizi

Suala la utambulisho unaohusu jinsia, hasa kwa wanawake, limevutia umakini wa watafiti, wasomi, na watunzi katika nyanja mbalimbali za kiusomi zinazochunguza mitagusano, maingiliano, na mahusiano ya kijinsia katika jamii. Hata hivyo, bado hakuna mwafaka wa pamoja kuhusu utambulisho wa jinsia. Suala hili limechunguzwa kwa lengo la kufichua dhuluma, kutosawa, au masuala mengine hasi yanayowakumba wanawake. Pamoja nachangamoto wanazopitia wanawake.Aidha, watafiti wa kiakademia wamechambua kazi za fasihi katika tasnifu zao katika viwango mbalimbali vya elimu, kama vile uzamili na uzamifu katika vyuo vikuu. Hii inaonyesha kuwa suala la utambulisho wa kijinsia linashughulikiwa aidha katika uandishi au utafiti. Kauli hii inaunga mkono mtazamo wa Wamitila (2002) kwamba fasihi ni kioo cha jamii kinachoakisi uhalisia wa maisha katika jamii rejelewa.Pia, inaweza kusemwa kuwa tungo hizi zinajenga utambulisho wa kijinsia ambao una mipaka finyu kati ya masuala ya kijinsia na masuala ya wanawake. Kwa mfano, tafiti nyingi zimeshughulikia suala la kijinsia katika fasihi ya Kiswahili.Watafiti kama Chesaina (1987), Lugano (1989), Muindi(1990),Mule(1991),Momanyi(1998),Swaleh(2011),naKamwara(2016) wamechunguza masuala kama usawiri na majukumu ya wahusika, mgongano kati ya usasa na utamaduni kwa mwanamke, pamoja na uchanganuzi wa masuala ya kijinsia katika tungo

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

mbalimbali. Hata hivyo, hakuna utafiti wowote uliochunguza masuala ya kijinsia kwa mtazamo wa uhusiano kati ya mitazamo ya watunzi na makuzi ya wahusika wanaowasawiri.

**Lengo Kuu**

Kutambua namna utambulisho wa jinsia ya kike unavyojitokeza katika tamthilia teule.

**Malengo Mahususi**

i. Kuchanganua utambulisho wa jinsia ya kike kisanii katika tamthilia teule.

ii. Kuchunguza athari za mazingira katika utambulisho wa jinsia ya kike katika tamthilia teule.

iii. Kubainisha athari za mitazamo ya watunzi kwa utambulisho wa jinsia ya kike na upembezwaji wa mwanamke katika tungo za tamthilia teule.

**Muhtasari wa Tamthilia ya *MamaEe***

Tamthilia hii ina sehemu mbili kuu. Sehemu ya kwanza ina maonyesho manne huku sehemu ya pili ikiwa na maonyesho matatu. Kwa jumla tamthilia hii inamaonyesho saba.

Katika sehemu ya kwanza,onyesho la kwanza linatukia sebuleni kwa Bw.Kinaya.Kuna mgogoro baina ya wahusika wakuu,Kinaya na Mwavita.Chanzo cha mgogoro huu ni kuwa Mwavita alikawia kumfungulia mumewe Kinaya.Mwavita anmfungulia mumewe mlango kisha kumtazama pasi kumchangamkia.Mwavita vilevile anakosa kumpa chakula kisa na Kinaya amerejea alfajiri baada ya usiku wa manane.Pia Mwavita anamnyima Kinaya fursa ya kumtazama mwana wao Juma kwa sababu Juma alikuwa analala kwani alikuwa mgonjwa.Mwavita vilevile anamweleza Kinaya kuwa hawajibiki katika ndoa,hajali wanachokila wao,pesa zake zinaishia kwa mahawara.Pia Mwavita anamkumbusha kinaya kuwa dada zake wanazurura mjini ovyo kama mbwa koko.Hili ni baada ya Kinaya kumweleza Mwavita kuwa dada yake Tenge ni hawara. Hatimaye Kinaya anamchapa Mwavita vibaya sana hadi kupoteza meno, anajipita hospitalini akiuguza majeraha.

Katika onyesho la pili,nje ya nyumba ya Mzee Tembo masahibu ya Tenge yanasadifiana na ya dada yake Mwavita.Tenge,msichana mwanafunzi wa umri wa miaka kumi na sita afurushwa shuleni kisa na maana ana ujauzito ambao alipachikwa na George ambaye ni mwanafunzi mwenzake.Japo suala hili ni gumu kwake Tenge ,George haonekani kuathirika nalo.Mgogoro unaibuka hapa kuhusu kufukuzwa kwa Tenge shuleni na mimba aliyonayo.Tenge na mama yake wakiwa katika hali ya kuvutana baba anawasikia na kisha mambo haya yanachukua mkondo tofauti.Tenge anachapwa na baba yake barabara.Mama anapiga nduru na kaka yake Tenge anajitokeza kwa ghafla na pindi anataarifa yaliyojiri,bila hata stahamala anashirikiana na baba yake kumwadhibu Tenge.

Katika onyesho la tatu,nje ya nyumba ya Mzee Tembo mnafanyika kikao cha wazee ambao wamekuja kusikiliza kesi ya Mwavita na mumewe Kinaya.Baraza hili lajumuisha aila ya Mwavita kwa mkono mmoja na Kinaya kwa mkono mwingine.Upande wa aila ya Mwavita wanalalamika kwamba awali walipowalaki aila ya Kinaya waliotaka kuomba radhi kisha wamrejeshe Mwavita kuishi na Kinaya hawakuonyesha heshima ambayo wakwe walistahiki kama ilivyo desturi za mila kwani walitukanwa na mkutano ukavunjika.Aila yake Kinaya wakubali kukosa na hatimaye wakatozwa faini ya fahali mkubwa,mbuzi dume,blanketi moja kubwa na mitungi miwili kubwa ya tembo kwa wazee.Faini hii inakataliwa na aila ya Kinaya kwani ilionekana kuwa kali mno.Hatimaye upande wa aila ya Mwavita walikubali kupunguza iwe fahali,blanketi na mtungi mmoja wa tembo.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Njeru Karimi Stella, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

Katika onyesho la nne,sebuleni kwa Kinaya,Mwavita hajihisi vizuri.Dada yake Tenge aingia na kusikitikia hali ya Mwavita.Hali ya mwili ya Mwavita ni hatihati.Hutapika kila anapojaribu kutia chakula mdomoni..Kinaya anawasili na kutaka kuenda shereheni na mkewe ambaye hajajiandaa kwa hilo.Kuna kuwa na mvutano baina ya Kinaya na Mwavita hatimaye Kinaya anaamua kuondoka lakini anaapa kuwatafuta wasichana wengine shereheni kwani Mwavita amekataa kuandamana naye.Katika hali hii Kinaya anagundua kuwa nguo zake hazijapigwa pasi.Kinaya anamsomea shemeji yake Tenge.

Katika sehemu ya pili,onyesho la kwanza,sebuleni kwa Mwavita.Awali ni Mwavita na Tenge tu ndio wamo ndani.Kidogo Mama anawasili na analakiwa kwa namna yake.Mama anazidi kuwapa wanawae mawaidha na anabidiika kuwatia moyo na azma ndio waweze kuikabili changamoto za dunia ipasavyo.Muda si muda Padre akiwa na sare zake rasmi awasili.Kuwasili kwa Padre kunazua mvutano baina ya Padre na Mwavita kuhusu suala na mume na mke kuwa kitu kimoja wakioana.Mwavita anaonekana kupinga njia zozote anazozitumia Padre kumshawishi kurejea kwa mume wake.Vilevile Padre anamweleza Mwavita kuwa haruhusiwi kusihriki meza takatifu kwa kuwa ni mwenye dhambi,amekataa kumsamehe mume wake..Hili linamfanya Mwavita kufichua unafiki wa Padre wa kujifanya mwokovu mchana na usiku ashiriki dhambi na mahawara.Hili linamkasirisha Padre na kumfanya kuondoka kwa kasi kiasi cha kusahau Biblia yake.Mama ya Mwavita na Tenge vilevile anaendelea kuwaonya kuwa waangalifu na kujifunza kutokana na masahibu yaliyowapata mbeleni.

Onyesho la pili,sehemu ya pili,mahakamani ,kesi ya talaka ihusuyo Mwavita na Kinaya imo mikononi mwa uamuzi wa hakimu.Wakili wa Mwavita na Kinaya wanakabiliana mbele ya Hakimu.Wote wanakubaliana kwa kuidhinishwa kwa talaka lakini wanatofautiana kwa matakwa yanayoandana na talaka.Kuna mgongano baina ya sheria za kienyeji na zile za Kiingereza.Sheria za Kiingereza kama zisomwapo na wakili wa Mwavita zinaelekea kumpa mwanamke tumaini katika hatua za kupigania ukombozi huku za kienyeji zikidumaza hatua hii.Kwa mujibu wa sheria za Kiingereza mtoto atasalia mikononi mwa mama mzazi kama hajafikisha umri wa miaka kumi na sita.

Katika onyesho la tatu na la mwisho katika sehemu ya pili,sebuleni kwa Mwavita,Mwavita na Tenge wapiga gumzo kuhusu namna George alivyoonekana kutaka kumrejelea Tenge katikati mwa mji kwa lengo la kutaka yule mtoto wao Jasiri.Katika kiserengerenyuma hiki Tenge alivutana mno na George.Mwishowe George alisalimu amri lakini baada ya kumtukana Tenge.Tenge atetewa na Kheri na Kheri ndiye anampoesha Tenge wakati anataka kuendelea kujibizana na George.Baadaye hawa kina dada wawili wanazungumzia juu ya Kheri.Kheri anasawiriwa kama mmoja kati ya wanaume elfu.Kheri ni mwanaume asiye na ubwana.Kheri ajua kuwa mke ni mtu kama yeye.

**Utambulisho wa Wahusika wa Jinsia ya Kike katika Tamthilia Teule**

**Mwanamke Sawa na Thamani ya Vitu**

Wanajamii wa jinsia ya kike hutazamwasawa na rasilmali na familia yake. Yaani pindi anapofika umri wa kuolewa yeye huozwa kama bidhaa sokoni. Familia ya mume mtarajiwa hulazimika kutoa mahari kwa njia mbalimbali, kwa mfano ng`ombe, mbuzi, kuku, mazao ya shambani, pesa na kadhalika.

> ***KINAYA***:..*Mwanamke hana chake. Akishaolewa kila kitu hata yeye mwenyewe ni mali ya bwanake. Ndiyo sheria ya kikwetu wacha uzungu hapa.*
>
> ***MWAVITA***:*…yaani ukilipa mahari umemnunua mtu! (uk.5)*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X)
*Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*


Kauli hii ya Kinaya inaweka bayana namna mwanamke wa Kiafrika anavyothaminiwa, hana lake pindi akishaolewa. Huchukuliwa kama mali ya mume na hivyo yuko chini yake. Itambidi kujinyenyekesha hata ikiwa yale anayotendewa ni maovu.

**Mwanamke kama Mtumwa wa Mwanaume katika Ndoa**

Kulingana na Beavoir (1985) jukumu la mwanamke aliye katika ndoa ni kupiga deki, kufua na mambo mengine kama hayo. Hata hivyo, jitihada za aina hii hazifai chochote kwani kila uchao zitatekelezwa. Mwanamke katika ndoa ni sawa na mtumwa katika hali zote. Hana uhuru wa kufanya maamuzi yoyote yale japo ya kimsingi. Suala hili linadhihirishwa na mwandishi hivi:

***MWAVITA***:...*Nione mimi! Sina uhuru wowote kila nifanyalo lazima likubaliwe namwenyewe. Sina msaada kutoka kwake. Hakuna tofauti kati ya mtumwa namimi. (Kimya kidogo.) Ndiyo iko tofauti moja ndiyo iko…Mtumwa huwa anajuwa kuwa yeye ni mtumwa lakini mke hajui kuwa yeye ni mtumwa!*

***TENGE***:*(Ambaye alikuwa akimsikiza dadake kwa mshangao.) Aah! Dada Mwavita sikujua kama una uchungu namna hiyo. Umeona dhiki hadi kutamani kuwa pahali pangu pa aibu! Unajipa utumwa! (Uk 60)*

Vilevile suala hili pia linadhihirika katika ndoa ya wazazi wake Mwavita naTenge, baba yao anamnyima mama yao ruhusa ya kuwatembelea. Hukuni sawa na kuwa mtumwa. Kulinganana tamaduni nyingi za Kiafrika, pindi mwanamke anapoolewa uhuru wake basi kamwachia mwanaume. Mwandishi anasema hivi:

***MAMA***…*Nawe Mwavita leo mimi nimekuja baada ya kumrai babako anipe ruhusa, Siku nyingi alikataa kwa kuwa ulirudi kwa bwanako kabla malipo…(uk.80)*

Kauli hii ya Mama yake Tenge na Mwavita ni ya kuvunja moyo kwa msichana anayepalia kujiingiza katika asasi hii ya ndoa. Kwani atalazimika kuupoteza uhuru wake wa kimsingi na kukubali kuishi chini ya huruma wa mwanamume ambaye ndiye mtoa maamuzi.

Tenge pia anamweleza Mwavita kuwa wanawake walio vijijini wanapitia hali ngumu zaidi kuliko walio mjini hususan kutokana na kutokuwa na elimu ya kutosha, hivyo basi wamegeuzwa kuwa watumwa. Kauli hii inabainika hivi:

***MWAVITA***: *Walio vijijini wana ufadhali.*

***TENGE***: *Waliovijijini ndio wana taabu zaidi. Hawajasomasana kwa hivyo wao wafanyishwa kazi kama punda. Walime mashambani wawaletee chakula mabwana walio mijini, wao ndio baba, ndio mama wa watoto wao. Wazae, walee, wauguze, waadhibu. Kila kazi juu yao. Huku mabwana hapa mjini wana wake waliowaweka. Wakumbuka mara moja moja tu kupeleka pesa nyumbani.*

**Mwanamke kama Mpokezi wa Tamaduni Potovu katika Ndoa**

Kulingana na Collins na Anderson (2006), ndoa hutokana na watu wawili kukubaliana kuishi pamoja wote wakiwa ni wa jinsia tofauti. Wanasema pia ndoa inaweza kufasiliwa kama muungano kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa baina ya wahusika wa jinsia ya kike na kiume waliokubaliana kuishi pamoja kama bibi na bwana.Hii inafutia hali ambapo Kinaya baba yake amelitelekeza suala hili kwa kujihusisha na unywaji wa pombe kupindukia. Suala hili linabainika katika kesi pale mahakamani hivi:

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

***WAKILI WA KINAYA***:*(Asimama na kumwinamia hakimu kwa heshima.) Labeka bwana-nitaendelea.*

Kufuatana na sheria za kiasili watoto siku zote ni wa baba hata kama hawajazaliwa bado. Mzeewa tatu alitweleza kuwa mtoto kamwe hawi ni wa mama na kuwa siku zote mtoto huenda na babake wazazi wakitalikiana. Baba aweza hata kuchukua mtoto anayenyonya… (uk 103-104)

**Mwanamkekama Malaya**

Umalaya au ukahaba kama anavyoeleza Muindi (1990:23),ni kitendo cha mwanamke au mwanamume kushiriki mapenzi na mwenzake kwa matamanio ya kufaidika kihali na mali.Akimnuku Dirasse (1978:15) anasema:

Malaya katika muktadha wa Kiafrika ni tofauti. Msichana yeyote aliyeonekana akiandamana mara nyingi na wanaume au wavulana, yule alichukuliwa kuwa malaya. Pia msichana aliyepata mimba na kuzaa kabla kufunga ndoa aliitwa malaya.

***KINAYA***:*…Kuna mahawara mji huu zaidi ya dadako Tenge! Ati mwanafunzi! Bila shaka nawe ungekuwa kama yeye ningekawiya kidogo kukuowa. Shukuru nilikuowa mapema(uk.9)*

**Athari za Mazingira katika Utambulisho wa Jinsia ya Kike katika Tamthilia Teule**

Huwa ni jambo la umuhimu kutalii mandhari ya utunzi wake mwandishi ili kumfaulisha msomaji wa kazi hii ya fasihi katika kichocheo cha mtunzi huyo kuamua kuwatambulisha wahusika wake jinsi alivyofanya. Kuna aina mbalimbali ya mazingira ambayo huweza kuathiri uandishi wa mtunzi katika utambulisho wa wahusika wake: kiwakati, mahali, na kidini. Masuala haya yameathiri mtunzi katika utambulisho wake wa wahusika wa jinsia ya kike kama ifuatavyo:

**Dini**

Dini imeondokea kuwa jukwaa ambalo linamdhalilisha mwanamke huku likimtukuza mwanaume. Kutokana na hili, mwanaume amepata msaada wa kuendelea kutowajibika kwani dini imemweleza kuwa mwanamke aliumbwa na Mungu kwa minajili ya kuwa msaidizi wake hapa duniani. Padre anaenda pale nyumbani kwa Mwavita na kujaribu kumrushutisha kurejea katika ndoa na mumewe Kinaya jambo ambalo Mwavita analikataa.

Kulingana na mazingira haya ya kidini ya mtunzi, mwanamke anafaa kuwa mnyenyekevu, mtii amri za kidini licha ya kutendewa maovu na jamii yake kwa kisingizio cha dini. Hili linabainika katika dondoo hili:

***PADRE***: *(Akichukua chai na kuanza kunywa huku akisema aweka Bibilia yake mezani.) Asante mama, huyu mwanao nimesema naye siku nyingi miezi kadhaa lakini ni mkaidi kama Wayahudi walivyokuwa waliposemeshwa na kuonywa na manabii hapo kale.*

***MWAVITA***: *(Amdakiza padre.) Lakini maisha ni yangu mwenyewe sheria ya Mungu yasema, `Usiue` yaani mimi mwenyewe sina madaraka ya kujiua. Sivyo…*

***PADRE***: *Ndiyo kujinyonga ni dhambi kubwa sana!*

***MWAVITA:*** *Sasa Padre, mtu akitaka kuniua name nisikimbie ningoje tu aniue si sawa nakujiua?*

***PADRE***: *(Akimwambia mama.) Unaona mama! Ndivyo asemavyo siku zote. Haishi maswali na mambo mengi ya kuhalalisha kitendo chake kiovu cha kuivunja ndoa ya Mungu.*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

***MAMA**: Lakini Padre huonikuwa Kinaya aweza kumuua. Wewe ulimwona hali yake ilivyokuwa. Hujui kuharibu mimba ni kifo? (uk.83-84)*

Naye Mama yake Mwavita anamweleza Padre hivi:

***MAMA:**...Mwanangu ungekuwa na mke kama huyu siku moja akutilie sumu katika chakula lakini bahati nzuri uponee chupuchupu. Akiomba msamaha umsamehe. Baada ya muda arudie tena kufanya hivyo ungefanyaje?*

**Wakati**

Mwandishi hulazimika kuakisi uhalisia huu kiwakati katika utunzi wake.Hali pia inajitokeza katika tamthilia ya *Mama Ee* (1987), mtunzi ameathirwa na mazingira ya kiwakati katika utambulisho wake wa wahusika wa jinsia ya kike. Hili linathibtishwa hususan katika lugha anayotumia kumtambulisha mhusika wa jinsia ya kike. Kwa kawaida lugha anayompa mwandishi mhusika fulani ili kuitumia katika kumtambulisha mhusika mwenzake huwa ni mtazamo wake mtunzi na jinsi angependa mhusika huyo kuonekana na wasomaji wa kazi yake.Hili linaweza kuthibitishwa na jinsi babake Tenge pamoja mwanawe wa kiume wanapomshtumu Tenge.

***KAKA**:(Kwa hasira anarukia fimbo na kumpiga Tenge.) Nilikukanya na hilo George lako. Faida gani umepata sasa? George anasoma bado na wewe je? Ulijiona umesoma sana husikii unayoambiwa. Hawara mkubwa we. (Amchapa fimbo. Mama ajaribu kumwokoa Tenge lakini achapwa kofi na kusukumwa na mumewe. Aanguka kwenye debe la maji. Yanamwagikakwakelele. Mamana Tenge wanalia.)*

Ni ukweli kuwa Tenge amewavunja wazazi wake moyo kwa kuenda kinyume na maelekezo aliyokuwa amepewa na kwa bahati mbaya akaweza kupata ujauzito wake George jambo ambalo linasababisha yeye Tenge kuambiwa na usimamizi wa shule kuwa nafasi yake haipo tena pale shuleni kwani ashakuwa mama. Lakini lugha anayotumia baba yake dhidi yake ni dhalilishaji na yenye ukali wa aina yake hususani ikiwekwa kwenye mizani ughuruba alionao baba na binti yake. Lugha anayoitumia baba dhidi ya binti yake ni wazi mwanamke hana lake katika jamii yenye mfumo wa kuumeni.

**Athari ya Mtazamo wa Mtunzi kwa Utambulisho wa Jinsia ya Kike na Upembezwaji wa Mwanamke katika Tamthilia Teule**

Utambulisho wa mwanamke unaojitokeza katika tamthilia ya *Mama Ee* ni kiwakilishi cha mtazamo wa mtunzi ambao kwa njia moja ama nyingine unatokana na jamii yake kuhusu nafasi ya mwanamke wakati huo. Mtazamo huu unajitokeza kwa njia zifuatazo:

**Uongozi wa Chama cha Umoja wa Wanawake**

Kulingana na Mwavita uongozi wa chama hiki ni wakutiliwa walakini. Chama hiki ambacho kinafaa kuwasaidia wanawake kuyakabili matatizo yao unadhihirisha ubaguzi wa aina yake. Wasimamizi wake wanakataa kuwasaidia wanawake wenzao kwa kusema kuwa wao hawawezi kupingana na mahakama. Mwavita anamkumbusha Tenge jnisi walioenda katika ofisi za chama hicho na hawakusaidiwa.Mwavita anasema hivi:

***MWAVITA**: Hukumbuki siku ile tulipoingia ofisini kwao tukidhani kuwa tutapata msaada mara moja. (uk.124)*

Ni wazi kuwa mengi ya matatizo yanayomkumba mwanamke yana chanzo chake kutoka kwa wanawake wenyewe. Tendo la wakuu wa chama cha Umoja wa Kina Mama kukataa kuwasaidia Mwavita na Tenge ni wazi kuwa udhalimu dhidi ya mwanamke utaendelea

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

endapo hulka ya baadhi ya wanawake walio na uwezo wa kuwasaidia wanawake wenzao hautabadilika hii ni kulingana na mtazamo wake mtunzi.

***TENGE****: Ungekuwapo ungefikiri nchi hii hakuna kina mama maskini. Nilishangaa.Maana asilimia tisini ya kina mama hapa nchini wako vijijini wengine hata hawajaingia garini.*

***MWAVITA****: Walipoanza kuzungumza ndipo tulipojuwa kuwa hicho chama ni cha kina mama waliosoma na walio katika tabaka la juu. Hawajui kabisa taabu za kina mama vijijini, kutembea maili kumi kutafuta maji! Wao walikuwa wakizungumza juu ya vitanda vibovu katika hospitali ya kuzalia kina mama hapa mjini na wakungawajeuri! Kijijini je? Hakuna hospitali, hakuna wakunga licha wakunga wajeuri? (uk.125)*

Kile kinachobainika katika dondoo hili ni kuwa wanawake walio na nafsi ya kuwakombolea hadhi wengi wa wanawake wanaopatikana vijijini hawataki. Wamejitenga nao na hili linadumaza juhudi kuupiga vita mfumo kandamizi dhidi ya mwanamke.

**Mwanamke kama Mjeuri**

Mtunzi anamsawiri mhusika mwanamke kuwa mjeuri. Japo taswira hii ni kinyume na jinsi mtunzi anatazamia kuonyesha jinsi mwanamke anavyoteswa na mwanaume. Kupitia kwa dhuluma anayopitia Mwavita, msomaji wa kazi hii anamwonea huruma ila kupitia kwa mtazamo wa mtunzi, ni wazi kuwa dhuluma na matendo ya kinyama anayotendewa mwanamke, mwanamke mwenyewe ndiye anayechangia hali hii. Wakati Kinaya akiwa mbele ya wazee kuezea sababu inayomfanya kupiga mkewe Mwavita, Kinaya anajitetea kwa kusema kuwa mkewe huwa anachochea hamaki zake kwa ujeuri wake. Inasemekana huwa anamtusi mara kwamara. Hii inabainika katika dondoo hili:

***MZEE WA KIJIJI****: Kinaya, una lolote la kusema juu ya haya yote yaliyosemwa juu yako? Lazima ujitetee.*

***KINAYA****:…Pia Mwavita alikuwa mjeuri sana kwangu ndiye aliyenitia wazimu wa kumpiga, Mwavita hanishemu mimi kama mumewe. Nikifika nyumbani usiku hufungua mlango tu akarudi kitandani, haniulizi nimekula nini wala hajali. Nikimwambia nataka atazusha ugomvi tuishie kupigana.*

Kupitia dondoo hili mtunzi anakuli kuwa kuteswa na kupigwa kwa wanawake kutokana na ujeuri wao na wala si ukatili wa waume zao.

**Muhtasari wa tamthilia ya *BembeayaMaisha***

Tamthilia ya *Bembea ya Maisha*ina sehemu nne, sehemu ya kwanza ina onyesho tatu, ya pili nne, ya tatu onyesho nne na ya nne onyesho tatu. Kwa jumla tamthilia hii ina onyesho kumi na nne.

Sehemu ya kwanza, onyesho la kwanza linatukia kwakeSara, Saraamepumzika kwenyekochi baada ya kumeza tembe alizopewa hospitalini. Yonaambaye akitzamwa vizuri ni mwingi wa uchovu na hasiraanajitosa ndani ya nyumba. Katika mwanzo wa onyesho hili tunapewa taswira kamili ya mhusika Yona ambaye anaonekana kukasirishwa na takribani kila kitu katika nyumba yake.Kulingan na Yona,Sara alifaa kumpa Neema taarifa kuwa alikuwa akiugua na hivyo alifaa kuja kumplekea hospitalini ili kuweza kupata matibabu.Wazo hili la Yona linapuuziliwa mbali na Sara ambaye anaeleza kuwa Neema ana aila yake ambayo alifaa kuipa nafasi ya kwanza Wazo lake Sara linaibua kutoelewana baina yake na mume wake Yona kuhusu wana wao.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

Onyesho la pili linafanyika katika nyumba yake Dina mwanawe Kiwa amewasili kwa lengo la kufahamu hali ya mama yake Dina.Dina anampa Kiwa taarifa ya jinsi aila yake Sara na Yona ilivyokuwa imedhalilishwa na jamii kwa kipindi kirefu kwa sababu ya kutojaliwa wana na pindi walipopata watoto,watoto hawa walikuwa ni wa jinsia ya kike ,tukio hili linasababisha wanajamii kuendeleza kejeli dhidi yao kwani hawakuweza kujaliwa na mtoto wa jinsia ya kiume ambaye kwa mujibu wa jamii hii angerithi fimbo ya baba yake.Kutonaka na kusemwa huku,Yona anatafuta jinsi ya kuondokea hili kwa kunywa pombe ambayo inamfanya kuwa mwingi wa vurugu ambazo alizielekeza kwa mke wake Sara.Onyesho hili linaisha kwa kuonyesha Dina akimuaga Kiwa ili kuenda kumsaidia Sara kumpikia mumewe Yona kwa sababu Sara ni mgonjwa.

Onyesho la tatu linafanyika jikoni mwake Sara.Dina amewasili na yupo katika pilipilika za kuandaa chakula kwa ajili ya Yona mumewe Sara.Sara amejilalia kwa sababu ya maumivu.Chakula kinapokuwa tayari,Sara anamshukuru Dina kwa kuwa alikubali kuja kumwauni.Dina anazipokea shukrani zake Sara na vilevile anamtia moyo ili aweze kukabili hali yake ambayo ilikuwa ikimsibu.Dina anamfahamisha Sara kuwa matukio mengi katika maisha yanatokana kudhura za Mwenyezi Mungu.Anamkumbusha vilevile kuhusu faraja aliyonayo kwani watoto wake licha kuwa ni wasichana wameweza kupiga hatua za kipekee katika maisha yao.

Sehemu ya pili, onyesho la kwanza linafanyika kwakeNeema, Neemana mama yake Sara wapo sebuleni. Sara ameletwa na Neema mjini ili kueza kumpeleka hospitalini kupokea kutibiwa ugonjwa wa moyo uliokuwa ukimtatiza. Neema anaonekana kuwa mwingi wa wasiwasi kwa sababu ya kukawia kurejea kwa mwanawe Lemi kutoka shule. Bela ambaye ni mfanyakazi katika nyumba yake Neema anamweleza Neema kuwa Lemi amekawia kufika nyumbani kwa sababu anashiriki katika maandalizi ya hafla itakayofanyika shuleni mwao ambayo kulingana Bela , Neema haikumbukuki kutoka na shughuli zake chungunzima.

Onyesho la pili linafanyika nyumbani kwake Neema.Neema ana mazungumzo na Bela ambaye ni mfanyakazi wake wa nyumbani.Katika mazungumzo hayo suala la changamoto ya maisha ya kisasa linabainika hususani kule kutangamna baina ya wazazi na watoto kumekuwa ni nadra saba hivi kwamba suala hili linazidi kuwa kero kwa wazazi..Katika onyesho hili pia,mwandishi anabainisha kuwa imekuwa ni vigumu kwa Neema na Lemi kutagusana kwa kuwa wakati anaporejea nyumbani Neema,Lemi huwa tayari keshalala.Katika onyesho hili pia nafasi ya mila za Kiafrika linabainika hivi kwamba Sara anadhibitiwa na mila hii kwa kutoruhusiwa kulala kwa mwanawe aliyeolewa.

Onyesho la tatu linafanyika nyumbani kwa Neema,mumewe Neema,Bunju yu tayari kufika kazini asuhuhi hiyo japo kunatokea gumzo baina yao kuhusu suala la matokeo ya Lemi ambaye ni mtoto wao.Kwa upande wake Neema ameridhishwa na matokeo hayo ila kwa upande wake Bunju anamtaka Lemi kujitahidi zaidi.Neema anamweleza Bunju kuwa mama yake tayari yupo mjini kwa ajili ya matibabu.Bunju anaonekana kutokuwa tayari kumwauni mke wake kwa kumpa hela ili aweze kushughulikia suala la matibabu ya mama yake.

Onyesho la nne linatokeakatika nyumba yake Asna pale mjini. Asna anamwandalia mama yake Sara staftahi. Sara anastaajabishwa na jinsi bintiye anavyoishi katika kidogo kama hicho. Asna kwa upande wake anajitetea kwa kusema kuwa chumba hicho kinapatikana katika eneo la watu walio mali zao na kwa hviyo anakifurahia chumba hicho. Kwa mujibu wa Sara, watu mjini wapo katika harakati za kuzumbua riziki ambayo daima huwa haitoshi. Asna ana mawazo tofauti na ya mama yake,

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X)
https://ijojournals.com/
Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
*Njeru Karimi Stella, **


Sehemu ya tatu,onyesho la kwanza linatokea katika nyumbaya Neema na Bunju.Neema yupo katika hatua za kunadhifisha nyumba mara anajipata kuwa mwingi wa fikra kuhusu ugonjwa na mama yake na jinsi ulivyomfukarisha.Akiwa katika hali hii,mumewe Bunju anajitoma chumbani pasi na Neema kuwa na habari,jambo hili linamfanya Neema kushtuka.Kwa awamu nyingine tena Bunju anakataa kumpiga jeki mkewe ili aweze kushughulikia matibabu ya mama yake.

Onyesho la pili linatokea hospitalini,Sara amelazwa .Neema na Asna wamewasili kwa kusudi la kumjulia hali.Sara anang`ng`ania kutaka kuondoka hospitalini na kurejea kijijini kwa gharama ya matibabu inazidi kuwa ghali kila uchao. Vilevile anataka kuondoka pale hospitalini ili kurejea kijijini na kuweza kumwauni mumewe Yona ambaye kwa sasa anataabika katika kuzitekeleza shughuli zote za nyumba.

Onyesho la tatu linafanyika nyumbani kwa Neema,Neemaanamwelekeza Lemi katika masomo yake.Lemi anatoa lala zake kuwa hajakuwa akipelekwa matembezi na wazazi wake.Licha ya Lemi kusema hivyo,Neema anamtaarifa waziwazi kuwa hataweza kumpeleka katika matembezi hayo kwani alikuwa na miadi ya kumpeleka nyanyaye Lemi kule kijjini.Lemi kwa upande wake vilevile anaonekana kuwa mwingi wa masuali kuhusu kufeli kwa nyanya yake kuja kumjulia hali.

Onyesho la nne lianfanyika nyumbani kwa Asna,kuna mazungumzo baina ya Asna na mama yake Sara.Kile kinachojitokeza katika haya mazungumzo ni kuwa Asna ana mtazamo hasi kuelekea suala la ndoa hivi kwamba amefikia uamuzi wa kuishi hivyo japo umri wake ushatimia wa kuingia katika asasi hii.Pili  ni kutokana na mateso ya aliyoyapata mama yake katika ndoa.Hivi kwamba,kuugua kwake Sara kunatokana na kupigwa na Yona katika ndoa.Kutokanaa na mifano hii ya ndoa zilizo na matatizo mengi.

Sehemu ya nne,onyesho la kwanza linafanyika nyumbani kijijini kwa Luka.Luka amewaalika Yona na Beni kuja kujipa raha kwa sababu ya mazao aliyoyapata shambani.Beni anakuwa na fursa ya kuwaeleza wazee wenzake jinsi kizazi cha sasa kinavyotupilia mbali mila zao hivi kwamba kizazi cha baadaye hakitakuwa na mila na desturi hizi.Katika mazungumzo ya wazee hawa watatu kile kinachobainika ni kuwa kizazi cha sasa kinaona kuwa kuishi kama mzungu ndiko kustaarabika.

Onyesho la pili linatokea nyumbani kwa Sara ,kijijini.Sara na Neema wanazungumzia suala la utamaduni na jinsi jamii inavyobadilika kila uchao.Kulingana na Neema ni kuwa dunia inapiga hatua kwa njia ya kasi ilhali kuna baadhi ya wanajamii ambao wanaendelea kunywa pombe kupindukia pasi na kulifahamu hili.Sara kwa upande wake anaonekana kuwa mtetezi wake Yona ambaye alitelekeza kazi za nyumba na mifugo vilevile.

Onyesho la tatu, linatokeaasubuhi kijijini kwaYona, Yona anaonekana akiwa pekee yake pale sebuleni. Ni mwingi wa mawazo na majuto kuhusu ugonjwa wa mkewe Sara.Anajutia jinsi alivyoishi maisha yake ya awali ambayo yalitokea kuwa kisababishi cha ugonjwa wa Sara.Akiwa katika hali hii Neema anampata. Yonaanastaajabishwa na jinsi binti yake alivyokata uzani. Yona anampa Neema shukrani zake kwa kujisabilia na kugharamia matibabu ya Sara mke wake.Katika tamati ya onyesho hili,Yona anamsihi binti yake Neema kumsamehe kwa kila kosa alilowatendea wakiwa wangali wachanga.

**Utambulisho wa Jinsia ya Kike Kisanii katika Tamthilia Teule**

Mwanamke wa Kiafrika ametwezwa huku mwanamume akikweza takribani katika asasi zote za kijamii. Jambo hili basi limewashurutisha watunzi wa kazi za kisanaa kutumia lugha

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

kupigania hadhi ya mwanamke. *Bembea ya Maisha*ni utungo wa kusukwa kisanii ambao unaibua suala la mgongano wa utamaduni wa kale na kisasa.

Umaduni wa kale unawasilishwa na wanajamii ambao wanapingana kwa namna yoyote ile jitihada za kumkweza mwanamke katika jamiii kama vile Beni huku wa kisasa unawasilishwa na wapenda mabadiliko katika jamii kama vile Neema, Asna, Sara na Dina.Mtunzi wa tamthilia ya Bembea ya Maisha amemtambulisha mwanamke kwa njia mbalimbali.

**Mwanamke kama Mwenye Akili Pevu.**

Tunaelezwa kuwa licha ya Sara na Yona kusemwa sana na wajamii wenzao namna ilivyo na Waafrika wanaopenda kujishughulisha na masuala yasiyowahusu waliweza kujaliwa watoto wasichana ambao walikuwa na fikra pevu na bongo za sumaku. Neema alisoma hadi Chuo Kikuu na kuweza kupata kazi ambayo inamwezesha kumlipia dada yake karo. Vilevile kugharamia matibabu ya mama yake Sara.Kwa mujibu wa Dina akimweleza Kiwa, Sara na Yona maisha yao ni kama filamu hadi mtu akielezwa hawezi kuamini kutokana na ufanisi walio nao na ambao umeletwa na mwana wao Neema.Dina anasema hvi:

> ***Dina****: …Tulivyo Waafrika, ikawa kuna waliojua tatizo kuliko wenye tatizo. Kazi ikawa ni kuwasema; wakalaumiwa na kusutwa. Watu wakanong`ona na kusema faraghani. Haikuwa rahisi kwao. (Kimya.) Lakini hatimaye Mungu akaridhia wakati wake aliouona bora. Vilaika vyao hivyo vikaja kujaliwa kuwa watu wazima; na kama kuvifidia vikapewa fikra pevu na bongo za sumaku. (uk.7)*

**Mwanamke kama Msomi**

Elimu huwa ni ujuzi anaopata mwanadamu wakati anaposoma. Mwanadamu anapopata elimu huwa anazipanua fikra zake na pia kupata uhuru wa kufanya maamuzi sahihi kutokana na maarifa aliyoyapata. Elimu ni kitu pekee ambacho mwanadamu hawezi pokonywa hapa duniani ila tu hadi kifoni. Ni rasilmali ambayo mzazi akimrithisha mwanawe huwa na uhakika kuwa itadumu milele. Neema mhusika mkuu anajukumika na kuwasomesha dada yake Asna hadi akawa na digrii. Vilevile Salome anasoma hadi Chuo Kikuu na kupata daraja ya kwanza katika shahada yake. Hili linasababisha wahisani kujitole kugharamia elimu yake tena nje ya nchi ili kumwezesha Salome kupata shahada ya pili.

Suala hili linabainika kupitia kauli hii:

> ***Bunju****:…Kumbuka nilikuachia mshahara huo ukamsomeshea Asna mpaka ana digrii yake ingawa bahati ya ajira haijamfungulia milango. Salome naye nimemlipia karo shule ya upili nachuoni. Kwa bahati nzuri masomo yamemwitika akapita vizuri na hiyo First Class.Amesihi nasi hapa akisoma hadi pale alipobahatika kupata ufadhili wa kwenda kuendeleza masomo yake ng`ambo…(uk.28)*

Msichana ambaye amezaliwa katika jamii nyingi za Kiafrika mara nyingi huwa katika hatari ya kuozwa mapema na jamii yake ili asije akawafedhehesha wazee wake kwa kuzaa akiwa nyumbani.Kwa msichana kama huyu,elimu ndio silaha pekee itakayomwepusha na udhalimu kama huu.Hivyo basi,msichana anapopata elimu mara nyingi wakerekewa wa masuala ya kijamii huliona hili kama tukio la sudi njema yaani kupitia kwa msichana huyu jamii yaweza kubadilika.

Vilevile, kupitiakwa elimu Neema anapata kazi ambayo inampa uwezo wa kuwasaidia wazazi wake kifedha, anagharamia matibabu ya mama yake Sara jambo ambalo kulingana na Kiwa endapo mama yake Dina angekuwa mgonjwa yeye kama mwanamume anageliweza.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Njeru Karimi Stella, *
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

**Mwanamke kama Mwajibikaji**

Sara anamkumbusha Yona kuwa Neema amekuwa akiyatekeleza majukumu ambayo si rahisi. Amewafaa wanuna wake kwa hali na mali kwa kuwalipia elimu ya Chuo Kikuu.

***Sara**:…Lakini huyo mtoto naye pamoja na mzigo wa familia yake amejaribu kwa kiasi chake. Amewafaa wanuna wake kwa hali na mali. Ninasikia kulipia elimu ya chuo kikuu si lelemama. Jambo hili limewashinda hata wanaume wenye mishahara minono serikalini. (uk.2)*

Licha ya hayo, Sara pia anamweleza Yona kuwa ugonjwa ambao anaugua haungembakisha endapo kama si Neema kuja kumpeleka kwa wataalamu.

***Sara**: Ugonjwa huu usingenibakisha hata nikaiona leo hii. Ulikuwa umenila kiasi cha kuniacha chichi; chichi kavu kwenye mwako wa jua. Hadi akaja yeye na kunipeleka kwa wataalamu. (Kwa sauti ya chini yenye huzuni.) Leo nisingekwako…(uk.2)*

***Yona**:(Kwa ukali.) Kubwa gani alilonifanyia?*

***Sara**: Yona, umesahau mara? Hukumbuki kuwa Neema alituajiria wafanyakazi kutusaidia…(uk.3)*

**Athari za Mazingira katika Utambulisho wa Jinsia ya Kike katika Tamthilia Teule**

Mtunzi wa tamthilia ya *Bembea ya Maisha* ni mzawa wa eneo la Nyanza nchini Kenya ambako kwa kiwango kikubwa jamii imepiga hatua hususan katika elimu ya mtoto wa kike ambayo inamkombolea hadhi kijamii japo kuna vizingiti ambavyo vinazidi kutweza hatua hizi za kuonyesha mabadiliko katika kumtambulisha mwanamke.Hata hivyo, kuna baadhi ya masuala ambayo yamo katika mazingira ya mtunzi yanayolemaza juhudi za kuonyesha mabadiliko katika utambulisho wa wahusika wa jinsia ya kike. Masuala hayo ni kama yafuatayo:

**Ubaguzi**

Ubaguzi ni hali ya upendeleo katika jamii. Hali hii uendelezwa kwakuzingatia kama vile; jinsia, tamaduni na kadhalika. Suala hili linashuhudiwa katika jamii kila uchao hususani ubaguzi wakijinsia. Yaani jamii nyingi za Kiafrika huwaweka mbele wanaume huku ikiwatweza wanawake. Wanaume ndio hudhaniwa kuwa waendelezaji ukoo, warithiwa mali ya familia. Na endapo familia haiwezi kumpata mtoto wa kiume huonekana kuwa na kasoro.

Ulevi huu unamfanya Yona kuwa mtu rafu na mwenye kupenda vurugu,anakuwa na mahudhurio mabaya kazini na hili linapelekea kufutwa.Dina anamweleza Kiwa hivi:

***Dina**:…Watu walimtia Yona maneno kuwa lazima awe na mrithi. Walimtaka aoe mke atakayemzalia watoto wa kiume kwa kuwa, kwa maneno yao, Sara alikuwa ameshindwa. (uk.9)*

Ni wazi kuwa mtoto wa kiume atazidi kupewa nafasi ya kwanza huku wa kike akiwa wa pili.Kwa kawaida mtoto ni mtoto tu,hakuna maana ya kuwapa wengine hadhi huku wengine wakionwa kama si watu.Suala la jinsia ya mtoto,mama mara nyingi hana uwezo juu yake,ni maumbile na kudhura za Mwenyezi Mungu lakini mwanamke hulaumiwa kwa hili.Japo mwanamke huyu ana uhuru wa kuondoka katika ndoa hizi dhalilishi,suala la kuacha watoto wake kulelewa na mwanamke mwingine huwa ndicho kikwakzo,kwa hivyo wanawake kama hawa huishia kumwomba Mungu kuwakirimia mtoto wa kiume ili wazidi kuishi na waume zao.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella*, *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*


**Ndoa**

Ndoa ni mojawapo ya asasi ya kitamaduni inayodidimiza juhudi za ukombozi wa mwanamke wa Kiafrika.Asasi hii huu huwa na misingi katika uwezo walio nao wahusika wa jinsia ya kiume wa Kiafrika ambao humpa nguvu na kiburi cha kumtazama mwanamke kama chombo na kitu kisichokuwa na thamani yoyote ile. Ndoa nyingi katika jamii za Kiafrika huonekana kuwa ni za kudumu endapo mwanamke atamzalia mumewe watoto na ikiwa hili halitokea basi mwanamke ndiye wa kulaumiwa na kusutwa na wanajamii kwa kuitwa tasa. Mtazamo huu mara nyinigi uakisiwa na watunzi katika kazi zao. Arege ameliakisi hili kupitia kwa mhusika Sara.

Sara aliolewa na Yona lakini kwa muda mrefu walikosa watoto, na kutokana na hili Yona alisemwa sana na wanajamii na mwishowe alijiingiza katika ulevi ili kuondokea bughuda hizi. Ulevi huu unamfanya Yona kugeuka kuwa mtu mwenye vurugu nyingi kwamkewe. Alikuwa akimpiga vibaya sana. Kutokanana kupigwa huku Sara anapata ugonjwa wa moyo. Hili linabainishwa kupitia dondoo hili:

***Dina**: Yaani yamesemwa amengi siku nyingi kama ilivyo ada katika jamii nyingi za Kiafrika. (Anaketi.) Asiyejua safari ya Sara na Yona akielezwa huiona kama filamu. Kwaufupi, Yona alifunga uchumba na Sara na hatimaye wakaoana na kuishi vizuri ila milango ya baraka ya watoto ikakawia kufunguka. TulivyoWaafrika, ikawanikuwasema; wakalaumiwa na kusutwa. Watu wakanong`ona na kusema faraghani. Haikuwa rahisi kwao. (Kimya.)*

*Lakini hatimaye Mungu akaridhia wakati wake aliouona bora. Vilaika vyao hivyo vikaja kujaliwa kuwa watu wazima; na kama kuvifidia vikapewa fikra pevu na bongo za sumaku. (uk.7)*

Mwanamke husemwa vibaya na wakati mwingine kutengwa na kuonekana kuwa mwenye laana au hata baadhi mbaya. Jambo ambalo si kweli kulingana na sayansi.

***Kiwa**: Ulikuwa unasema kero za watu hazikuishia pale.*

***Dina:** Nilikuwanimesahau. Naam, hazikuishakamwe. Watu walimtia Yona maneno kuwa lazima awe na mrith aoe mke atakayemzalia watoto wa kiume kwa kuwa, kwa maneno yao, Sara alikuwa ameshindwa. (uk.9)*

***Kiwa**:…Aisee!*

***Dina**:…Pamoja na ulevi wake, Yona alianza kumpiga Sara; tena kipigo cha mbwa hasa alipokuwa amelewa. Mara kadhaa alimwagiwa maji baridi kumrejeshea fahamu.*

***Kiwa**: Kwa nini kichapo chote hicho?*

***Dina**: Eti hakumzalia mtoto wa kiume…(uk.10)*

Kutonaka na kauli hizi, ni wazi kuwa jamii ya Kiafrika inapomwona mwanamke kashinda kumzalia mume wake watoto wa kiume, humlazimshwa mwanamume huyu kuoa mwanamke mwingine ili amzalie watoto wa kiume.Licha ya Yona kufahamu kuwa mkewe Sara alikuwa akiugua kutokana na maradhi ya moyo aliyomsababishia kutokana na kichapo cha mara kwa mara bado Yona anamtaka Sara kumshughulikia kwa kumpikia chakula. Hili linabainika kupitia dondoo hili:

***Yona**: Sara, bado ungali pale pale? Nyumba hii haifuki walau moshi hata kama chakula ni taabu kwako? (uk.1)*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

Wanawake wanaopatikana vijijini katika jamii nyingi za Kiafrika huwa ndio wapokezi wakuu wa mateso anayopitia mwanamke kwa sababu ya jinsia yake. Wao hufanywa kuwa watumikizi wa mwanaume. Wanafaa kuwapikia, kuwafulia na kuwazalia na kuwalelela watoto. Wakati mwingine kwa kuwa wanawake hawa pia ni wanadamu na wanaweza kuwa wagonjwa, wanaume wao huwashurutisha kutekeleza masula haya basi na kufahamu kadhia yao. Halini sawa na utumwa.

**Athari ya Mtazamo wa Mtunzi kwa Utambulisho wa Jinsia ya Kike na Upembezwaji wa Mwanamke katika Tamthilia Teule**

Kwa mujibu wa Rimmon-Kenan (1983), mtazamo ni jinsi ambayo utungo unaweza kupewa maana yaani ni yale mambo yanayotuwezesha kuumba maana kutokana na namna msimulizi wa hadithi anavyoyaweka matukio yake anayoysimulia.

Hivyo basi katika kazi hii tumedhihirisha namna Timothy Arege alivyowapa baadhi ya wahusika wake majina kama njia mojawapo ya mtazamo wake juu ya wahusika wa jinsi ya kike kama ifuatavyo:Basi akamwingilia Hajiri, naye akapata mimba, bibi yake alikuwa duni machoni pake.Hali hii pia inadhihirika katika maisha ya Sara na Yona kama inavyobainika katika dondoo hili:

***Dina:****…Asiyejua safari ya Yona na Sara akielezwa huiona kama filamu. Kwaufupi, Yona alifunga uchumba na Sara na hatimaye wakaoana na kuishi vizuri ila milango ya Baraka ya watoto ikakawia kufunguka.*

*Tulivyo Waafrika, ikawa kuna waliolijua tatizo kuliko wenye tatizo. Kazi ikawa nikuwasema; wakalaumiwa na kusutwa. Watu wakanong`ona na kusema faraghani. Haikuwa rahisi kwao. (Kimya.)*

*Lakini hatimaye Mungu akaridhia wakati wake aliouona bora. Vilaika vyao hivyo vikaja kujaliwa kuwa watu wazima; na kama kuvifidia vikapewa fikra pevu na bongo za sumaku.* (uk.7)

***Dina****: Kusema nako walisemwa. Lakininilivyosema, Mungu hamwachi mja wake. Aliitikia sala zao kwa wakati aliouona bora.*

***Kiwa****: Wajuaji wakabaki vinywa wazi.*

***Dina****: Hata! Afadhali hiyo wazi. Walivifumba haswa ndiyo maana hukulisikia mpaka hivi lilivyonitoka kinywani. (Anamtazama usoni.) (uk.8)*

Kile kibainika hapa ni kuwa mtunzi ana mtazamo chanya dhidi ya mhusika mwanamke, jamii hii ina itikadi kuwa, mwanamke ambaye hajapata mtoto anatazamwa kama mwanajamii asiyefaa. Hivyobasi, mtunzi analibadili hili kwani Sara anapata watoto baada ya kipindi kirefu na hivyo hadhi kukweza kulingana na jamii yake. Suala la kupata mtoto lipo nje ya uwezo wa mwanadamu na ikiwa litakawia, haifai mwanamke kuwa ndiye wa kulaumiwa kwa hili.

***Dina****:…Faraja ni zao la dhiki. Leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago.*

*Kiwa: Kwa hivyo ameyapitia mengi?*

***Dina****: Tena mazito.*

***Kiwa****: Pamojana tabasamu zake? Ninajua amepitia mitihani kama familia yoyote ile ila kila nikikutana naye uso wake umejaa tabasamu. Hata hivi akiwa mgonjwa.*

***Dina****: Huyo ndiye Sara.Mmoja katika watu waungwana dunia hii.*

***Kiwa****: Sikujua alikuwa na lolote kubwa lililomkaa moyoni.*

***Dina****: Mwanangu nikwambie nini? (Kimya.) Sara ameitwa tasa. Wakati mwingine yeye na mumewe wameitwa wagumba, japo shoka la ugumba limemwangukia yeye zaidi kuliko mwenziwe.*

***Kiwa****: Lakini mama, si wana watoto? Au ndiyo unasema watoto hawa si wao?*

**IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH**
**(ISSN: 2805-413X)** ***Njeru Karimi Stella, ****
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.*

***Dina**: Damuyao hiyo lakini wameiona baada ya hodari wa kusema kuwabandika hili na lile.*
***Kiwa**: Vipi hivyo?*
***Dina**: Yaani yamesemwa mengi siku nyingi kama ilivyo ada katika jamii nyingi za Kiafrika…(uk.6-7)*

Kulingana na mtazamo wa mtunzi ni kuwa, ndoa haifai kuezekwa kwenye misingi ya kupata watoto pekee, inafaa kuwa pahali ambapo watu wawili mke na mume wataweza kuishi kwa amani bila mmoja wa wana ndoa hawa kuonekana ndiye mkosaji endapo katika ndoa hii hamtapatikana watoto.

**Neema**

Ni mwana wa Sara na Yona ambaye ni kifunguamimba,mkewe Bunju na pia mama yake Mina na Lemi.Sara na Yona wamempata baada ya kipindi kirefu tangu wafunge ndoa.Wanajamii wengi walikuwa wakikisia kuwa Sara alikuwa tasa.Japo Sara na Yona walipata watoto wengine baadaye ambao pia nao walikuwa ni wasichana,wanajamii hawakukomea pale kuwasema.Wengine walimtaka Yona kumwoa mke mwingine ili aweze kumzalia mtoto wa kiume ambaye angekuwa mrithi wake.Dina anamweleza Kiwa hivi:.

***Dina**: Mahasidi hawana sababu. (Kimya.) Halafu upo huo Uafrika mwanangu. Watu waliuliza na wangali wanauliza ardhi ya Yona atarithi nani!*

***Kiwa**: Kwa hivyo wanataka mrithi! (uk.8)*

Vilevile anawatafutia wazazi wake mfanyakazi wa nyumbani kwa sababu wazazi hawa umri wao unawafanya kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli.Mtunzi anadokeza hivi:

***Sara**: Lakini huyo mtoto naye pamoja na mzigo wa familia yake amejaribu kiasi chake. Amewafaa wanauna wake kwa hali na mali. Ninasikia kulipia elimu ya chuo kikuu si lelemama. Jambo hili limewashinda hata wanaume wenye mishahara minono serikalini.(uk.2)*

Mtoto msichana ana uwezo wa kuwasaidia wazazi wake jinsi alivyo mtoto wa kiume, cha msingi ni mtoto huyu kupewa fursa ya kupata elimu bora ambayo itampa uwezo wa kiuchumi wa kuyatekeleza haya basi na kuwa mtegemezi kwa mwanaume.

Pia kauli inadhihirishwa kupitia kwa mazungumzo baina ya Luka, Beni na Yona.

***Luka**:…Zamani mila zetu hazikuruhusu watoto wa kike kwenda skuli au kurithi kitu. Sasa wanakwenda nakurithi. Zamani watoto wa kike walikuwa wanategemea mifuko ya waume zao. Sasa hali nitofauti. Tamaduni, milana desturi zetu zinazidi kuyakubali mabadiliko. Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka. Kuyapuuza haya yote ni kazi bure.*

***Beni**: Watoto gani wa kike? Hawa wa Yona? Hebu wataje wengine.*

***Luka**: Si neno ni hao tu lakini si waiona tofauti? Watoto wetu wa kiume hawalinganishwi nao hata kidogo!*

***Yona**: (Amelewa kiasi.) Wala watoto wa kike na wa kiume hawalinganishwi.*

***Luka**:(Kwa Yona.) Sikiliza Yona.Watoto hao wanalinganishika sana. Kumbuka awali sisi tulidhani watoto wa kike si kitu. Tulijua akisha kukua ataolewa akuache. Unakumbuka tulivyokushinikiza kuoa mke mwingine upate watoto wa kiume?*

***Yona**: Ninakumbuka.*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

***Luka****: Afadhali hivyo ulivyofanya. Kumbe watoto hawa tuliowadharau walikuwa nyota ya jaha. Sasa kijiji kina mwanga.*

***Beni****: Mwanga?*

***Luka****: Mwangahaswa. (Kimya.) Mtoto alirudi hapa juzi ile nyingine akipeleka gari safi. Mimi nikashindwa nani huyu anaingia humu kwa sisi kina yahe na kulikubalia gari lake kutembea pasipo barabara ya maana! Kutazama nikamwona mtoto wetu, Neema, ameshikausukani. Unadhani nilikuwa na furaha kiasi gani? Sasa kila niendako ninawaambia watu tuna simba wa kike anayenguruma. (Wote wanacheka.) (uk.60-61)*

Mtunzi anadhamiria kuwa mtazamo hasi na wa kihafidhina dhidi ya mwanamke unafaa kutupiliwa mbali. Kulingana naye mtoto wa kike ni sawa na mtoto wa kiume, kwa hivyo anafaa kupewa fursa sawa mtoto wa kiume. Ana uwezo wa kuwasaidia wazazi wake, kurithi mali na hata kuendeleza ukoo wake.

**Hitimisho**

Utafiti huu umebaini kuwa licha ya mwanamke kupambana kutaka kujikombolea hadhi,kuna baadhi ya maswala ambayo yanadumaza hili,kwa mfano suala la utamaduni na mitazamo ya kijamii kumhusu mwanamke.Mwanamke mwenyewe kuwa kizingiti cha kujikombolea hadhi.Kwa mfano wale wanawake ambao ni wasimamizi wa chama cha kina mama ambao wanawabagua wanawake wengine.Vilevile dini inaendeleza dhuluma dhidi ya mwanamke kwa kumlazimisha kufuata baadhi ya kaida japo zinatishia maisha yake.

Mwanamke anayezaa watoto wa kike kusutwa na jamii yake na kuonekana kuwa hafai na hivyo mume waka analazimishwa na jamii yake kumwoa mwanamke mwingi ili aweze kumzalia watoto wa kiume. Anatia bidii kazini, anawasomesha dada zake na pia kuikimu familia yake. Vilevile imebainika kuwa elimu ndicho chombo muhimu anachoweza kukitumia mwanamke kujinasua kutoka katika utamaduni wa kijamii ambao umezidi kumdhalilisha. Pia imedhihirishwa wazi kuwa mwanamke pia ana uwezo wa kukataa kuishi chini ya udhalimu wa mwanaume.

Kwa ujumla utafiti huu ulibaini kwamba watunzi wa jinsia zote wanapinga dhuluma dhidi ya mwanamke. Hili linabainika kupitia kwa utambulisho wao wa wahusika wa jinsia ya kike. Watunzi Ari Katini Mwachofi na Timothy Arege wamefaulu kudhihirisha na kuihamasisha jamii dhidi ya dhuluma dhidi ya mwanamke. Kulingana na wao asasi kama ndoa, dini na utamaduni ndivyo vikwazo vikuu kwa ukombozi wa mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika.Tumeonyeshwa namna ndoa inavyolitekeleza hili na kuwasababishia wengi wao magonjwa.

***MAREJELEO***

Arege, T. (2022). *Bembea ya Maisha.*Nairobi: Access Publishers Limited.

Habwe,J.(1995).*Maumbile si Huja*.Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation.

Habwe,J.(2010) . *MaishaKitendawili*.Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation.

Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Fasihi*.Dar es Salaam:Press and Publicity Centre.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) *Njeru Karimi Stella,* *
https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
MABADILIKO KATIKA UTAMBULISHO WA WAHUSIKA WA JINSIA YA KIKE KATIKA TAMTHILIA: MIFANO KUTOKANA NA TAMTHILIA YA MAMAEE NA BEMBEAYAMAISHA.

Kezilahabi,E.(1971).*Rosa Mistika*.Nairobi:Kenya Literature Bureau.

Mohamed,S.A. (2010) .*Nyuso za Mwanamke.*Nairobi:Oxford Press.

Mwachofi, A.K. (1987). *Mama Ee*.Nairobi:Heinman Kenya Ltd.

Ndungo, C. (1985).*Wanawake na mabadiliko ya Kihistoria*, Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijajapishwa)

Ndungo,C.(1996).Uhakiki wa Fani katika Riwaya ya Katana Mkangi.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

TUKI:(2004) *KamusiyaKiswahiliSanifu*.Nairobi: Oxford University Press.

Steady, F.C. (1981).*The Black Women Cross-culturally.* Cambridge: Schenkam Publication

Taiwo,O.(1984).*Female Novelist of Modern Africa.*Lagos:Macm.illan Publishers.

Walibora,K.(2012).*NasikiaSautiyaMama*.Nairobi:East Africa Educational Publishers.